

# Pambazuko

Toleo Namba 071

Jumatatu Mei 6-12, 2024



## Bunge: Serikali inahujumu

UK. 18-19 **kilimo**

RC kugawa chai, urojo bure

UK. 14



Jicho la Tai

## Polisi wanawaogopa sana CCM

UK. 5

MCT

kupigania ubora habari za uchaguzi

UK. 7



Utata kifo cha Mkuu wa Majeshi Kenya



kutenguliwa UK. 10



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

**Mvua siyo tatizo, ni ubovu wa miundombinu**

**T**ANGU mwezi uliopita – wa Aprili, Tanzania imekuwa kwenye misukosuko inayotokana na mafuriko katika maeneo mengi nchini.

Wengi, ikiwamo serikali, wanasingizia kuwa kuwa kuharibika kwa miundombinu kunatokana na kuongezeka kwa kiwango cha mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Ni kweli mvua zimesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu huku maeneo mengine, kama ilivyo kwa Barabara ya Dar es Salaam-Lindi-Mtwara na wilayani Ifakara, kusombwa na maji na kuwepo kwa mafuriko.

Lakini, wakati wengi wakilaumu ongezeko la mvua kuwa ndilo jambo linalosababisha uharibifu huu, utalaamu unaonyesha kuwa madhara makubwa ya mvua hizi yanasababishwa na miundombinu hafifu ambayo haikujengwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi tunayoyashuhudia.

Pambazuko tunaamini kuwa nchi yetu ina tatizo kubwa la kutokuwa na mipango ambayo inafikiria nje ya kile tunachokifanya.

Mathalani, kama upembuzi uliofanyika wakati wa ujenzi wa barabara eneo la Jangwani, Dar es Salaam ungeangalia uwezekano wa kuongezeka kwa mvua, ungetoa jibu la aina ya barabara inayopaswa kujengwa hapo na leo tusingekuwa tunahangaika kuwahamisha watu kila mara ili kuboresha miundombinu katika eneo hilo.

Wajenzi wa reli ya kisasa (SGR) kati ya Morogoro na Dodoma, waliliangalia hili katika eneo la Msagali na Igandu ambalo kwa miaka kadhaa limekuwa likiathiriwa na mafuriko na huenda wakawa wamepata dawa.

Kwa mujibu wa maelezo ya wahandishi wa mradi huo usanifu wa eneo hilo umefanyika kwa kuzingatia takwimu za kiwango cha mvua zinazonyesha katika eneo hilo na kuongeza takwimu hizo ili hata kama ikitokea mvua zikaongezeka, basi reli hiyo isiathiriwe na mafuriko.

Hii ndio mipango inayopaswa kufanyika maeneo mengi nchini.

Sisi tunaamini kuwa kinachosumbua wala siyo ukubwa wa mvua, bali ni mipango mibaya ya ujenzi wa miundombinu yetu.

Ndio maana hata barabara zilizojengwa na kukamilika hivi karibuni na madaraja yake, zimeharibiwa na mvua zinazoendelea kwa sababu usanifu wake haukuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa.

Tumeshuhudia madaraja ambayo yanajengwa na kuwekewa makaravati wakati hata mtu asiye msomi wa ujenzi, anabaini kabisa eneo hilo linahitaji aina nyingine ya daraja.

Mfano mzuri ni Daraja la Kiyegeya katika Barabara ya Morogoro – Dodoma, tangu ukarabati umefanyika, daraja ambalo awali lilikuwa linasumbua kila mvua inaponyesha, hivi sasa hakuna anayelitumia licha ya nchi kukumbwa na mvua kubwa.

Aidha, wizi na ubadhirifu katika miradi vinasababisha kila mara tuwe na miundombinu ambayo ni hafifu na dhaifu.

Pambazuko tunasema kuwa wakati umefika sasa kuhakikisha kuwa wataalamu wanapewa uhuru wa kupanga aina ya miundombinu inayohitajika katika eneo fulani ili pale mambo yatakapoharibika tuwe na nguvu ya kuwahoji na pengine kuwashitaki.

## UTALII WA NDANI...



*Hoteli maarufu ya Essque Zalu Zanzibar, iliyoko eneo la Nungwi, Zanzibar, kama inavyoonekana nyakati za jioni. Ni mahali penye utulivu na mandhari ya kuvutia kwa wale wanaopenda kufurahi, kupumsika na kuhuisha akili baada ya majukumu mengi ya maisha. (Picha kwa hisani ya hoteli).*

### Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### NUKUU



*Bila taarifa sahihi, hatuwezi kukabili habari potofu na zenye uongo. Chombo huru cha habari, siyo chaguo, bali ni hitaji muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi na watu wake – Antonio Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN).*

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



## Polisi wanawaogopa sana CCM

Na Igo AI

**A**FYA ya Mzee Tai inaendelea kuimarika baada ya kukumbwa na changamoto kadhaa za mwili “kugoma kufanya kazi inavyotakikana.”

Mgomo huo wa mwili wa Mzee Tai unatokana na umri zaidi, ingawa na unyemelezi wa magonjwa ya hapa na pale.

Ni kutokana na sababu hizo za afya, kwa wiki mbili hakuwa na “makekeyake” ya kawaida, ambayo humlazimu mwandishi wake kuwepo kwenye ukurasa huu kila wiki, akiandika yale anayotaka yawafikie Watanzania na dunia.

Leo Mzee Tai kaamka akiwa na afueni, maana ameonekana mapema alfajiri, akizunguka- zunguka upenuni mwa nyumba yake, akiwa amevalia fulana yake maarufu yenye picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan. Fulana hiyo pia imebeba maandishi haya –“Mitano Tena kwa Mama.”

Mzee Tai kudamka kote huko, kumbe alikuwa anafanya mazoezi na baada ya muda alirejea sebuleni kuketi na kumuita kijana wake ili kumpa maelekezo ya kumwandalia staffahi.

Baada ya kustaftahi, Mzee Tai akaomba aitiwe mwandishi wake ambaye alikuwa chumba chenye televisheni ambako hushinda huku kukusanya habari zinazotangazwa ili kumsimulia yanayojiri duniani. Ifahamike kuwa Mzee Tai ana shida ya uoni.

Basi, mwandishi alipofika akaambiwa atafute namba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camillus Wambura kwani ana kazi nayo muhimu.

Namba ikapatikana na kupewa Mzee Tai, ambaye aliibofya kwenye simu yake ya ‘kitochi.’ Akabofya tena na tena, lakini ikasikika sauti nyororo kutoka upande wa pili kwamba “namba unayopiga, haipatikani kwa sasa.”

“Hivi hawa watu wa simu wanafanya



IGP Wambura

kazi gani, au na wewe umenipa namba isiyokuwa ya IGP Wambura, hebu ipige wewe kwa simu yako,” alifoka Mzee Tai baada ya kukosa kuwasiliana na mkuu wa jeshi la polisi.

Hakika mwandishi wa Mzee Tai akathibitisha kuwa namba ya IGP Wambura haipatikani, hivyo akashauri wajaribu baadaye, kwani huenda kiongozi huyo yuko kwenye kikao.

Baada ya muda mfupi, Mzee Tai akaanza kufoka tena; “hivi inakuwaje Jeshi la Polisi Tanzania linashindwa kazi, iweje hadi sasa yule kijana hajakamatwa na kutiwa ndani na angekuwa mahakamani, nini kimekwamisha sheria kuchukua mkondo wake?”

Mzee Tai akaendelea: “Hawa Polisi, tena wakiongozwa na mtu msomi kama Wambura wanashindwa kutekeleza majukumu yao na kumuacha mtu, tena kijana mdogo akitaka kuleta machafuko, tena anadai anapoteza watu, kwanini bado yuko uraiani?”

Akaongeza: “Najua jeshi limejaa watu wa waoga na wanaojipendekeza kwa chama changu cha CCM, lakini siyo haki, huyu kijana akamatwe.”

Kumbe anayezungumzia ni Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kagera, Faris Buruhan, aliyesema chama chake kinapoteza watu.

Mzee Tai bhana!

## Habari

## Hamad: Cuf haijafa, haifi kamwe

Na Mwandishi WETU,  
Dodoma

**C**HAMA cha Wananchi (CUF), kimetamba kuwa hakijafa na kujigamba kwamba kamwe hakitakufa.

Sababu za kutopotea katika uso wa siasa za Tanzania ni kwamba chama hicho “kiko moyoni mwa watu.”

Akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalum yaliyofanyika jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa CUF, Hamad Masoud Hamad, amesema dhana kwamba chama anachokiongoza kimekufa, “ndiyo mfu,” na wanaodai hivyo, hawajui siasa.

“CUF ni chama kikongwe, kinaheshimika na kiko ndani ya miyo ya Watanzania, hivyo anayedhani kimekufa, anajidanganya, na hakika hajui siasa za nchi yetu,” ameingeza Hamad.

Amesema kuwa ukubwa na ukuu wa CUF utadhirihi katika uchaguzi mkuu wa mwaka kesho, 2025, na kwamba matokeo ya kura “yatawashangaza wanaokibeza.

“Naomba niwahakikishie Watanzania, kupitia gazeti lako la Pambazuko, kuwa chama chetu cha CUF ni kikubwa mno na wengi wataona namna tunavyoendelea kuwa na mizizi ndani ya miyo ya watu wetu, wasubiri tu, wataona maajabu,” ameingeza katibu huyo mkuu.

Hamad akijibu tetesi kuwa CUF ‘kimekufa zaidi’ Tanzania Bara, amedai, chama hicho bado kina mizizi Mtwara, Lindi, Tanga na hata Kigoma, ambako amesema “wanaokiomba kife, wataona makeke yake.”

Kiongozi huyo amekiri kuwa kweli CUF ilipoteza nguvu zake baada ya “kukimbiwa na viongozi wa juu na wanachama wengi, na kujiunga na ACT-Wazalendo, lakini sasa wamegundua walikokimbilia, hakuna kitu cha maana, hivyo wameanza kurejea.

“Kweli watu wetu wengi walikimbilia ACT-Wazalendo kwa matumaini makubwa ya kupata haki na demokrasia zaidi, lakini



*Katibu Mkuu wa CUF, Hamad Masoud Hamad*

waliyokuta huko, hawakuamini na sasa wanarejea kwa makundi, nasi hatuna hiana, tunawapokea na kazi ya kujenga chama inaendelea,” amesema Hamad.

Kiongozi huyo anadai kuwa nguvu ya chama hicho kwa upande wa Zanzibar, bado ni kubwa na kueleza zaidi kwamba Kisiwa cha Pemba, na maeneo jirani, kimejikita zaidi na huku kinategemea kupata wawakilishi wengi wa wananchi baada ya kupata ushindi kwenye uchaguzi ujao.

Chama cha CUF kilikumbwa na mgogoro mkubwa wa kiuongozi ambao uliibua makundi mawili ya aliyekuwa katibu mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharrif Hamad (sasa marehemu) na mwenyekiti aliyekuwa akitambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Profesa Ibrahim Lipumba.

Baadaye Maalim Seif na viongozi wengine, waliamua kujiunga na ACT-Wazalendo na kumwachia chama Prof. Lipumba, ambaye anaendelea kuwa kiongozi mkuu wa chama.

Matokeo ya mgogoro huo yalionekana pia baada ya Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, Februari 18, 2019, kutengua uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wadhamini wa CUF wa kambi ya Prof. Lipumba.

*Soma mahojiano katika toleo la wiki ijayo.*

## MCT kuhimiza weledi habari za uchaguzi

Na Mwandishi WETU,  
Dodoma

**B**ARAZA la Habari Tanzania (MCT), limejizatiti kuchochea uwepo wa amani, utulivu na kuaminiana miongoni mwa Watanzania wakati wa mchakato wa uchaguzi ujao.

Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura amewahakikishia Watanzania kuwa baraza analoongoza litafanya kila linalowezekana kusaidia vyombo vya habari na waandishi wake kupata elimu, na ikiwezekana, uwezeshi katika rasilimali fedha ili kupata nyenzo za kufanya kazi kwa ufanisi wakati wa kuhakiki wapiga kura, kampeni, kupiga kura na kutangazwa matokeo.

“Tumesihuhudia mara nyingi wakati wa uchaguzi, vyombo vingi vya habari vinaandika kuhusu wagombea na kuacha kabisa masuala muhimu yanayogusa wananchi, hii inachangiwa na mambo mengi, sasa MCT inajipanga kuhakikisha mchango wa vyombo vya habari unaonekana na kuthaminiwa kwa umma,” amesema Sungura katika kongamano liliandaliwa na MCT na kufadhiliwa na Ubalozi wa Marekani.

Tanzania itakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu mwaka kesho, 2024.

Sungura amesema MCT itahakikisha inatoa elimu mahsusi kwa waandishi wa habari kabla ya uchaguzi wa mwaka huu na baadaye mwaka kesho, kuhusu uelewa mpana wa sera za kila chama na kuzifafanua kwa urahisi ili zisambae kwa wananchi na wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka.

“Vyombo vingi vya habari havina mpango kazi wa masuala ya uchaguzi, hili nalo tumeona ni mihumu na tutaweza kutoa mafunzo, kwa kutumia wazoe fu, ili kila chombo cha habari kiwe kinatambua kinafanya kipi, muda gani, kwa minajili ya



*Ernest Sungura*

nani,” amesema Sungura.

Sungura amesema vyombo vya habari vikitumika vyema kuandika, kutangaza na kuonyesha habari kwa weledi; haki, usawa na utu, ni hakika kuwa Tanzania itakuwa na uchaguzi wenye haki.

“Uandishi wa habari za uchaguzi kwa weledi, hujenga usawa, haki na uwajibikaji, na hapo ndipo tunataka mchango wa vyombo vya habari ufikie,” amesema katibu huyo mtendaji wa MCT.

Katika kongamano hilo lililofanyika Aprili 30, Jaji Joseph Sinde Warioba, waziri mkuu mstaafu, aliviasa vyombo vya habari kusaidia taifa kwa kufanya tafiti zitakazoisaidia serikali kutoa uamuzi wa kuendeleza nchi.

Warioba, ambaye pia ni makamu wa kwanza wa rais mstaafu, alionyesha kushangazwa na vyombo vya habari sasa kuandika na kutangaza zaidi habari za matukio bila kuwa na habari za kuelimisha.

Aliwataka wanahabari wasiwe sehemu ya kulalamika wakati wana nafasi kubwa ya kutengeneza agenda kwa kufanya tafiti na kutoa elimu ya mambo ya msingi kwa nchi.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Tanzania (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, wawakilishi wa mabalozi wa Uingereza na Marekani na waalikwa.

## Habari

## Hasham ashitaki Tanroad kwa Samia

Na Rashid MTAGALUKA,  
Morogoro

**M**BUNGE wa Ulanga, Morogoro, Salim Hasham amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan “kutumbua” wasaidizi wake wasiwajibika, huku akiinyoshea kidole Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads).

Hasham amesema hayo baada ya “kulilia” huduma ya Tanroads katika jimbo lake, kwa maelezo kuwa maisha ya wananchi yamekuwa magumu zaidi kutokana na kuharibika kwa miundombinu, na hakuna juhudi za wakala huo zinazoonekana kufikia eneo lake.

Amesema wakati huu wa mvua kubwa zinazoendelea, barabara nyingi za Ulanga zimeharibika na madaraja kusombwa, hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi.

“Kikubwa ni kwamba, hizi mamlaka ambazo zimewekwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, zimekuwa tatizo kubwa kwa sababu licha ya kutoa taarifa, watendaji wake hawataki kutimiza majukumu yao kwa wakati, jambo linalofanya wabunge na madiwani tuelekane hatutimizaji wajibu wetu kwa wananchi”, amelalama mbunge huyo.

Hasham aliendelea kusema kuwa, mvua hizo zimefanya kupanda maradufu kwa bei za bidhaa muhimu zinazotumiwa kila siku na wananchi ikiwemo gharama za usafiri.

“Mvua zimeleta maafa makubwa katika Jimbo la Ulanga, hususan katika miundombinu ya barabara, hivyo kusababisha umbali wa kilometa 68 tu, abiria kulazimika kulipa nauli kati ya Shilingi 40,000 hadi 60,000, badala ya Shilingi 10,000 zilizokuwa zikilipwa awali,” amengeza kwa masikitiko.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, kupanda kwa nauli kumefanya kuwepo ongezeko la bei za bidhaa kama vile



*Mbunge Salim Hasham*

chumvi iliyokuwa ikiuzwa kilo moja kati ya shilingi 300 hadi 500, na sasa ikifikia hadi Shilingi 3,000/; unga wa sembe ni Shilingi 3,000 kwa kilo na sukari sasa inauzwa hadi Shilingi 7000 kwa kilo.

Hasham amesema katika kipindi cha miezi minne mfululizo cha adha ya miundombinu ya barabara, hakuna mamlaka yoyote ya serikali ikiwemo Tanroads iliyowahi kutembelea Ulanga walau kutoa pole kwa wananchi walioathirika kwa maafa licha ya taarifa rasmi kuwafikiwa watendaji wa serikali.

“Ukiacha barabara, zaidi ya mashamba hekari 5,000 za wananchi wa Jimbo la Ulanga yamesombwa kwa maji, hiyo inasababisha kuwepo kwa tatizo kubwa la njaa, zaidi ya tani 500 za mazao tulizotarajia kuvuna mwaka huu, ina maana hatutaweza kufanikiwa, hivyo wananchi wanakwenda kupata adha kubwa ya njaa”, amebainisha.

Pambazuko litemfikia Meneja wa Tanroads Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Kyamba Alinanuswe kuhusu madai ya mbunge huyo na kukiri kuwepo kwa tatizo, huku akieleza kuwa maeneo mengi yameharibika, lakini yote yatafikiwa na kurekebisha.

Alinanuswe amesema kuwa kuwa mvua bado zinanyesha, yapo maeneo ambayo yatachelewa kidogo kurekebisha kwa kuwa kuwepo maji mengi kunakwamisha kazi kufanyika kwa ufanisi na kuwaomba wananchi wa Ulanga “kuvumilia kidogo.”





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Hawa ndiyo wabunge wetu, tusishangae!

Na Rashid MTAGALUKA

**T**ANGU mfumo wa vyama vingi vya siasa urejeshwe mwaka 1992, mwenendo wa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nao umebadilika.

Mwenendo umekuwa wa “mipasho zaidi” na kuacha hoja za msingi za kujenga na kupigania maslahi mapana kwa taifa letu, ambayo ni sababu kubwa ya kuwakilisha wananchi bungeni.

Watanzania wengi huku mitaani na kwenye mitandao ya kijamii wanashangaa na kutokwa mapovu kuwashambulia wabunge kwa kauli zao.

Nami nashangaa kwa sababu wabunge hawa hawakujipeleka bungeni, na wala hayupo yeyote miongoni mwa aliyeingia kuwa mjumbe akitokea mbinguni, hapana! Bali ni wabunge waliochaguliwa na sisi wananchi.

Hivyo, tunavyowaona wabunge wetu walivyo imara na wapole, wanavyojua kujenga hoja, wanavyotamani kujiongezea posho, huku wakipendekeza waliowachagua wakatwe kodi kwa kutumia simu, wanavyosifiana na hata wanavyojibizana, vyote hivi vinaakisi jamii iliyowachagua. Ndivyo Watanzania tulivyo!

Kwa mfano, tumewahi kusikia Mbunge wa Mtera (CCM) Livingstone Lusinde akisema ndani ya bunge; “kuna wabunge ambao wana mimba sizizotarajiwa bungeni...”

Watu wakastaajabu mheshimiwa kusema maneno hayo ndani ya bunge, lakini haukupita muda mrefu aliyekuwa Mbunge wa Kondoza Kusini (CCM), Juma Nkamia naye akasikika akisema “Sugu naomba unyamaze. Mimi ndiye nazungumza. Mimi siongei na mbwa, naongea na mwenye Mbwa.”

Siyo waheshimiwa wabunge wetu kutoka chama tawala pekee ambao



Bunge

Watanzania wamewahi kuwasikia wakizungumza na kuwashangaa, hata wale wengine wanaotoka kwenye vyama vya ushindani hawakubaki nyuma.

Mathalan kauli, “Udom (Chuo Kikuu cha Dodoma) kuna udini wa hali ya juu, wanafunzi wa dini tofauti hawalali chumba kimoja.” Aliyekuwa Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini, huku Mbunge wa zamani Viti Maalum (Chadema), Leticia Nyerere akisema; “Kwa kuwa wanaume wengi wanabaka, kifunguliwe kituo wafundishwe kutongoza.”

Yote tisa, 10 ni wiki iliyopita pale tulipomsikia Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Mohamed Said Issa akiitaka serikali kurejesha upya utaratibu wa watu wote wanaoingia Zanzibar kuwa na hati ya kusafiria.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2024/25, mbunge huyo alisema lengo ni kuvilinda visiwa hivyo.

Baada ya kauli hii wananchi wengi wakiwemo pia baadhi ya viongozi, walimshangaa wakidai hoja yake imejengwa kwenye misingi ya kibaguzi zaidi.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Selemani Jaffo alisema pamoja na maoni mazuri ya Issa, lakini hoja yake ni ya kuturudisha nyuma badala ya kusonga mbele.

Rashid Mtagaluka ni Mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu 0784 43 85 46 na barua-pepe: mtagaluka@gmail.com

## Kenya

## Tume kuondoa utata kifo cha Ogolla

NA Julius MKAMBI

**M**EJA Jenerali John Omenda ambaye ni Kamanda wa Kamandi ya Wanaanga nchini Kenya, amekabidhiwa jukumu nzito la kubaini chanzo kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Majeshi, Jenerali Francis Ogolla.

Ogolla alifariki dunia kwenye ajili ya ndege Aprili 18 mwaka huu na kuzua minong'ono.

Jenerali Ogolla na maofisa wengine tisa wa jeshi walifikwa na mauti wakiwa kazini wakitekeleza majukumu yao kufuatia agizo la Rais William Ruto la kulitaka jeshi kusimamia ujenzi wa shule, ikiwemo kutoa ulinzi kwenye maeneo ambayo yamegubikwa kwa matukio ya ujangili.

Maofisa wengine waliyopoteza maisha yao kwenye ajali hiyo ya ndege ni Brigadia Swaleh Saidi, Kanali Duncan Keitany, Luteni Kanali David Sawe, Meja George Magondu - ambaye alikuwa rubani, Kapteni Sorah Mohamed, Kapteni Hillary Litali, Sajenti John Mureithi, Sajenti Cliffonce Omondi na Sajenti Rose Nyawira.

Tume hiyo imeundwa ili kuweka wazi kilichosababisha ajali hiyo na kumaliza minong'ono, hususan kutoka kambi ya wanasiasa.

Wanasiasa hao wamekuwa wakihimiza kufanyika kwa uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo halisi cha ajali hiyo au kuwepo kwa hujuma.

Uteuzi wa Jenerali Ogolla Aprili 29 mwaka jana uligubikwa na shutuma za uwepo wake kwenye Ukumbi wa Bomas wa Kenya, jijini Nairobi ikidaiwa alikuwa miongoni mwa maofisa wa ngazi za juu walioшинikiza Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) kutomtangaza Ruto mshindi wa urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2022.

Rais Ruto alisema licha ya kufahamu alichokifanya Jenerali Ogolla kabla IEBC kutangaza matokeo ya mwisho ya urais, bado alimteua kushika wadhifa wa mkuu



Meja Jenerali John Omenda

wa majeshi akisisitiza alivutiwa na uzoefu pamoja na weledi wake kwenye masuala ya kijeshi.

Ruto alisema kabla ya kumteua Jenerali Ogolla alimuita kwa ajili ya mazungumzo na Ogolla alimwambia hana cha kujitetea na kwamba yeye (rais) alikuwa na uamuzi wa mambo matatu; kumpelekea mahakama ya kijeshi, kumstaafisha au kumsamehe.

Licha ya Rais Ruto kusema Jenerali Ogolla alikwepo Bomas kwa nia ya 'kupindua' matokeo, kiongozi wa upinzani anayewania uenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika, Raila Odinga, anasisitiza Ogolla alikuwa mtu mwadilifu asiyeweza kujaribu kushawishi matokeo ya uchaguzi.

Kauli hiyo ya Raila inaungwa mkono na Waziri wa Ulinzi, Aden Duale, aliyesema Ogolla ambaye wakati huo akiwa Makamu wa Mkuu wa Majeshi, uwepo wake katika ukumbi wa Bomas ulitokana na maelekezo ya mabosi wake japo yeye mwenyewe hakujuua nini alichokuwa anatakiwa kukifanya.

Kifo cha Jenerali Ogolla na matukio yaliyotokea ukumbi wa Bomas yanaibua maswali mengi, hivyo Meja Jenerali Omenda na timu yake ya uchunguzi inayoundwa na wanajeshi waliyoboea, wanatakiwa kuweka hadharani mbivu na mbichi kwa lengo la kuzima dukuduku la wananchi.

## Sasa Ikulu ivue ‘miwani ya mbao’

Na Elphaz CHARLES

**W**ATANZANIA wengi wanaamini kuwa siasa ni uongo, wizi, ufisadi na udikteta.

Dhana hii imejengeka kutokana na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wanasiasa wenyewe kuanzia kwenye vyama vyao hata wanapopata dhamana ndani ya serikali.

Kila mtu tayari moyo wake umeshajeruhiwa kupitia siasa, huenda ndiyo sababu wengi huamini kuwa siasa ni “mchezo mchafu.”

Kama siyo kujeruhiwa katika uongozi mbovu, basi ni katika upotevu wa mali za umma, ufisadi, ulaji rushwa, kucheleweshwa usuluhishi wa migogoro.

Migogoro hiyo ni kati ya wakulima na wafugaji, wananchi na wawekezaji, pamoja na kutolipwa fidia baada ya kubomolewa nyumba au kuchukuliwa ardhi.

Ni kwa sababu hizo na zingine nyingi, ndiyo maana ikitajwa siasa, kila mtu “kengere ya hatari” inasikika kichwani mwake.

Hata hivyo, maana halisi ya siasa ni mfumo wa maisha, uchumi, biashara, utawala katika jamii ambao watu wamekubaliana kuufuata ili kuishi kwa amani nap engine kwa usawa.

Tukirejea katika mfumo wa uongozi hapa Tanzania, siasa imechafuliwa na wanasiasa, kuna muda unaweza kuamini kuwa baadhi ya watendaji wa serikali ni vipofu au wamevalishwa miwani isiyoonna mwanga, hata ikiwa mchana.

Tanzania kuna mambo mengi ya ajabu yanatokea kila uchao. Mambo haya ni mabaya na yanaumiza umma, lakini hakuna kiongozi anayekemea, hivyo wananchi kuamini kuwa yanayotokea yana baraka zote za viongozi wa juu.

Mathalan, ubadhirifu uliothibitishwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye baadhi ya mashirika na taasisi. Lakini hakuna hatua yoyote ya kisheria inayochukuliwa, huku wahusika wakibaki wanatamba mitaani kwa



*Rais Samia Suluhu Hassan*

maisha ya kufuru kwa fedha za wizi na ubadhirifu.

Inashangaza kuona kuwa watendaji wengi wa serikali na taasisi zake, wanafanya kazi chini ya kiwango, na kuwa chanzo kikuu cha ubadhirifu unatokea.

Wananchi wanahoji, iweje haya yanatokea na viongozi wa juu - kuanzia waliomo Ikulu, na wasaidizi wao waaminifu wa ofisi hiyo kuu wanakaa kimya? Na kama wanachukua hatua, mbona wananchi, ambao ndiyo wenye Tanzania yao, hawaelezwi?

Wizara nyingi zimejaa ‘madudu,’ lakini hakuna anayeziwajibisha kwa hilo, viongozi wote sasa wako kimya.

Ni aibu kuona nchi ina viongozi wakuu wengi, ina vyombo vingi vya usalama, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa kukomesha rushwa na ubadhirifu, wala hakuna nguvu ya “wakubwa” inayoonekana dhahiri kukemea uzembe uliotapakaa kila ofisi ya serikali kwa sasa.

Hata hivyo, bado nina imani na Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba anaweza kuwa mwarobaini, ikiwa atakaza msimamo na kukana kauli yake ya “kila mmoja anakula kwa urefu wa kamba yake.”

*Mwandishi anapatikana kwa namba: 0685 872 763 na barua-pepe: elphazcharles@gmail.com*

## Afya

## Tezi-dume inapogeuka saratani

Na Mwandishi MAALUM

**T**EZI-dume siyo ugonjwa – kama inavyotambulika kwa wengi, bali kiungo muhimu katika maumbile ya mwanaume.

Kiungo hiki hupatikana katika mfumo wa uzazi wa mwanaume katika shingo ya kibofu cha mkojo.

Kazi yake kubwa ni kutengeneza majimaji ya uzazi kwa mwanaume, wengine wakiita manii, ambayo husaidia kurutubisha mbegu za kiume zilizotengenezwa kutoka kwenye korodani; na pia husaidia mbegu za kiume kubaki hai kwa muda unaostahili.

Kiungo hiki, hakina tatizo, lakini kubadilika kwa maumbile yake – hasa kutanuka, husababisha tatizo la afya, endapo tatizo hilo halitadhibitiwa mapema.

Umuhimu wa tezi-dume

Tezi-dume hutoa majimaji ambayo huchanganyika na mbegu za kiume na kutengeneza manii. Asilimia 60 ya manii ni majimaji yaliyotengenezwa na kiungo hicho, huku asilimia 40 ndio mbegu za kiume zilizotengenezwa kwenye kiwanda cha mbegu (korodani).

Majimaji yanayotoka kwenye tezi-dume hutangulia mbele wakati mwanaume anapofika kileleni wakati wa tendo la ndoa, na kazi yake ni kusafisha njia ya mkojo ili kuondoa asidi ili mbegu za kiume zisife.

Wataalamu wa viungo vya uzazi wanaeleza kuwa tezi-dume ndio yenye kufunga njia ya mkojo na kuruhusu mbegu za kiume zitoke wakati umefika kileleni na kuziba njia ya mbegu za kiume

na kufungua njia ya mkojo unapokuwa umemaliza tendo. Hii inafanya kutokuingiliana muda wa kutoa manii au kukojoa!

Pia, umuhimu mwingine wa tezi-dume ni kuchuja sumu na kuzuia zisichanganyike na mbegu za kiume na kuhakikisha usalama wa mbegu hizo.

Tezi-dume inapokuwa ugonjwa

Tezi-dume linapovimba ama kutanuka, hapo ndipo kile kinachoitwa ugonjwa hutokea na kuleta madhara makubwa ikiwamo shida ya kukojoa, kupata maumivu ya kibofu na hata kutokuwa na uwezo wa kuzalisha.

Ni vyema kuwa na mazoea ya kufanya vipimo vya mara kwa mara ili kujua hali za afya ya tezi-dume na afya ya viungo vya uzazi kwa ujumla.


Tezi-dume linapotanuka na kutochukuiwa hatua za kudhibiti kuongezeka kwake, husababisha saratani.

Saratani (kansa) hiyo ni pili kusababisha vifo vingi zaidi kwa wanaume baada ya saratani ya mapafu katika takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO).

Dalili za saratani hiyo ni pamoja na kukojoa damu, damu kwenye mbegu za kiume, maumivu ya mgongo na kukojoa kwa shida.

Wakati mwingine, dalili hizi za saratani ya tezi-dume zinaweza zisionekane mapema, hivyo ni vyema wanaume kupima mara kwa mara afya ya viungo vya uzazi – kwenye hospitali kubwa.

Wenye umri wa kuanzia miaka 45, wenye uzito mkubwa (wanene), ni rahisi zaidi kupata ugonjwa huo kuliko wenye umri mdogo na wenye miili ya wastani.



## Niko Dodoma kuchanganya dini na kilimo

Na Dkt. Benson BAGONZA

**N**IMEFIKA Jiji la Dodoma na kwa siku tatu nimekuwa nikifuatilia uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2024/25.

Mara nyingi nalaumiwa na baadhi ya watu kwa kuchanganya dini na siasa. Safari hii nimeamua kuchanganya dini na kilimo. Kwa nini?

Ileweke kuwa mimi ni mdau wa kudumu wa sekta hii. Baba yangu ni ofisa kilimo mstaafu anayepata pensheni chini ya laki. Mama yangu ni "Profesa" mstaafu wa kilimo asiye na pensheni.

Pia, dayosisi ninayoiongoza inamiliki na kuendesha miradi ya kilimo pamoja na chuo cha kilimo na mifugo (Karuco).

Dayosisi ninayoiongoza ni mwekezaji wa ndani katika sekta hii. Tumeanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata matunda; mradi wenye thamani ya Shilingi bilioni 5.

Watanzania wote, wema na wabaya, chawa na wazalendo, wenye dini na wanaodhani hawana, wote hawa, kila siku hula na kwenda choo kwa sababu ya kilimo.

Sasa bajeti yenyenye

Bajeti ni nzuri iliyojengwa katika maono makubwa kuliko wanaojadili. Zinahitajika jitihada kubwa kuziba mwanya mkubwa uliopo kati ya maono na uhalisia. Semina! Semina! Semina! Zisiwe na posho ndipo watasikiliza.

Bejeti ni kubwa kupata kutokea (ya Shilingi 1.2). Lakini mpaka Aprili 2024, bajeti inayomalizika imekwishapewa asilimia 53 ya fedha zilizoombwa mwaka jana. Natamani serikali iwape ili tutafute mchawi kwingineko.

Bado kuna mgongano kati ya wakulima halisi na wanaolima kwa kutumia simu (madalali). Biashara bila udalali ni ngumu. Usalama wa mkulima ni ushirika, lakini umejaa majizi. Kushughulika na majizi ni kazi ya wizara nyingi zisizoungana. Nani amsaidie mkulima dhidi ya madalali na majizi?



*Waziri Bashe akifurahia jambo na Askofu Bagonza.*

Maendeleo ya teknolojia ya kilimo yanaishia maofisini. Kazi ya kilimo iko vijijini. Washenga wa ofisi na wakulima ni maofisa ugani na vyyuo vya mafunzo. Bila hili, tutaendelea kufurahia maonyesho mazuri kutoka mashanva darasa, siyo kutoka kwa wakulima.

Sekta binafsi katika Kilimo inazungumzwa zaidi kuliko kutendwa. Vyyuo vya kilimo vimejaa wanafunzi kwa msongamano. Vyyuo vya sekta binafsi havina wanafunzi. Chakula hakina tofauti ya sekta binafsi na serikali. Tushirikiane, tusishindane.

Waziri wa sekta na timu yake wanaonyesha dhamera ya dhati. Wanahitaji ushirikiano. Kikwazo kimoja mbele yao ni ongezeko la rushwa katika taifa letu. Rushwa inaua matumaini ya taifa letu.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe anamudu nadharia za kiuchumi kutoka kambi kuu zote za kiuchumi duniani (Ubeperi na Ujamaa). uamuzi wake, vitendo vyake na uthubutu vinashawishi.

Kimsingi, Bashe ni mchumi kuliko wachumi wetu wengi. Ni mchumi sahihi kwa uchumi wa nchi inayotegemea kilimo, lakini ni rahisi kukwamishwa na wenye hulka za wivu.

Mwandishi ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe.

## Habari

## RC Unguja kugawa bure chai, vitafunwa

Na Jabir IDRISSA,  
Zanzibar

**M**KUU wa Mkoa (RC) wa Kusini Unguja, Zanzibar, Ayoub Mohamed Mahmoud amebuni kauli-mbiu ya kuchechea utendaji kazi ili kuleta ufanisi.

Kauli -mbiu hiyo aliyoipa jina la "Amsha-amsha Kusini," inalenga kuamsha ari ya kuchapa kazi baada ya kuona ufanisi serikalini unashuka siku hadi siku.

Ayoub anayejulikana mbunifu wa mbinu za kufanikisha jambo, ameeleza imani yake kuwa kauli-mbiu hiyo itafanya kazi na matunda yake kuonekana.

Akionyesha kuchoshwa na utamaduni unaozidi kukua Zanzibar kwa baadhi ya watumishi wa serikali kutumia muda mwingi wa kazi kwenda kunywa chai, kula mihogo ya kuchoma na urojo, sasa anataka kuwagawia chai yenye vitafunwa wakiwa ofisini.

RC Ayoub ameliambia Pambazuko kuwa atagawa chai ya kiwango cha juu, kwani itahusisha mkate uliopakwa siagi na vitafunwa vingine ili kudhibiti utamaduni wa wafanyakazi kutoka kila wakati kwa kisingizio cha kwenda kunywa chai.

"Nitaanza Jumatatu ya tarehe 6 Mei, na sitatoa pesa hii kwenye mfuko wa serikali," anasema RC Ayoub, mtaalamu mbobezi wa uhasibu.

Akifafanua ili kuonyesha alivyoamua kujitolea kuchagiza ufanisi na utendaji kazi wenye tija katika mkoa wenye raslimali nyingi za kiuchumi kama vivutio vya utalii vikiwemo makazi ya pomboo walioko Ghuba ya Menai, kijijini Kizimkazi; kimapunju waliozagaa kwenye Msitu wa Jozani kijijini Pete, RC Ayoub anaweka bayana, "Sitatoa pesa kwenye mfuko wa serikali kutekeleza mpango huu. Nitaugharamia kwa kutumia mshahara wangu."

Mkuu huyo wa mkoa analalamika kuwa utamaduni huo umekuwa



Ayoub Mohamed

"ukila muda mwingi wa kazi" na ukichanganya na kadhia mpya simu janja (Smartphones) zinazotumika kupata taarifa mchanganyiko zikiwemo za wasanii, michezo mbalimbali, tamthilia na hata michezo ya watu wazima, imekuwa tatizo sugu linalokwamisha utendajikazi wenye tija.

Anasema utamaduni huo umekuwa ukizorotesha kazi na kuchelewesha kuhudumia wananchi na wageni wanaotaka huduma mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji unaotegemewa kuinua pato la taifa na kuiwezesha serikali kutoa huduma za jamii zenye ubora.

Pamoja na kujaaliwa raslimali nyingi hizo za kiuchumi, mkoa huo unajulikana ulivyo nyuma kielimu kwa kuwa na idadi ndogo ya vijana wanaosoma ama kumaliza vyo vya elimu ya juu.

Mkoa huo pia una vyo vikuu viwili; Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ambako kampasi ya Taasisi ya Utawala wa Umma (IPA) vipoTunguu.

Hata hivyo, mkoa huo unaoendelea kuwa na bahati ya kutoa viongozi wa kitaifa wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) akiwemo Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwenyekiti wa sasa wa chama hicho.



# *Tangaza na* **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au  
Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

**Makala****Serikali iache 'blabla' ilipe vyombo vya habari**

Na Mwandishi WETU,  
Dodoma

**S**UALA la madeni makubwa ya serikali kwa vyombo vya habari lilifanywa kuwa rasmi yapata miaka mitatu iliyopita katika mkutano mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) uliofanyika mjini Morogoro.

Katika hotuba yake ya ukaribisho, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile alimweleza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi, kuwa serikali ni moja ya taasisi ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuvifanya vyombo vya habari kuwa hoi bin taaban kiuchumi.

Balile alisema vyombo vingi vya habari vinadai fedha kwa taasisi mbalimbali za serikali baada ya kuvipatia huduma - nyingi zikiwa ni huduma za matangazo, lakini taasisi hizo hazijalipa madeni hayo.

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu Majaliwa aliviagiza vyombo vya habari kuandaa taarifa inayonyesha ni chombo gani, kinadai taasisi gani ya serikali na kiasi cha fedha kinachodaiwa.

Baada ya kutoka Morogoro, kazi hiyo ikafanyika na taarifa kufikishwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Vyombo vya habari vikakaa kusubiri kulipwa. Lakini malipo hayakufanyika kama ilivyotarajiwa.

Baada ya hapo suala hilo likaanza kuwa ajenda katika vikao vya taasisi mbalimbali za kihabari. Inaelekea serikali ikaona kuwa suala hilo ni kubwa. Yakatolewa maagizo kuwa ufanyike uhakiki wa madeni hayo ili yale yatakayokidhi vigezo yalipwe haraka.

Baada ya hapo tukasikia maagizo kutoka viongozi wa serikali kuzitaka taasisi zake kulipa madeni ya vyombo vya habari.

Kwa kuwa bado taasisi za serikali zinahitaji huduma za vyombo vya habari, ilitarajiwa kuwa taasisi ambazo zitatumia huduma hizo zitalipa huku zikiendelea kupunguza madeni ya awali.



**Waziri Mkuu Kassim Majaliwa**

Lakini, katika mkutano mwingine mkuu wa mwaka wa TEF uliofanyika Lindi mwaka jana, 2023, Balile akiwa bado ni mwenyekiti wa TEF na Majaliwa akiwa mgeni rasmi kwa mara nyingine, Balile akarejea suala hilo na kubainisha kuwa hali imezidi kuwa mbaya kwani madeni hayo badala ya kupungua yameongezeka.

Hiyo inamaanisha kuwa hata kama kuna taasisi zililipa sehemu ya madeni hayo, lakini taasisi nyingi siyo tu hazikulipa, bali ziliendelea kupata huduma za vyombo vya habari na kutolipa madeni mapya.

Inaonekana bado msisitizo huo haukusaidia kwani kwenye mkutano wa 13 wa kitaaluma wa TEF mwaka huu uliofanyika jijini Dodoma wiki iliyopita ilielezwa kuwa madeni hayo yamekuwa na sasa yamefikia kiasi cha shilingi bilioni 18! Ilidhaniwa kuwa madeni haya yangukuwa yanapungua badala ya kuongezeka!

Katika mkutano wa mwaka hii, mgeni rasmi alikuwa ni msaidizi namba moja wa waziri mkuu, yaani Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Biteko.

Naye akatoa maelekezo kama yaliyowahi kutolewa mara kadhaa awali na bosi wake, kuwa taasisi za serikali zilipe madeni hayo.

Hakukuwa na kipya sana kuhusiana



## **Serikali iache ‘blabla’ ilipe vyombo vya habari**

*Inatoka Uk. 16*

na suala la ulipaji wa madeni zaidi ya kuhimiza yalipwe. Labda kilichobadilika ni maneno yaliyotumika kufikisha ujumbe huo.

Halikadhalika, hoja hiyo ya madeni ya serikali kwa vyombo vya habari ikatawala hata katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani ambayo nayo yalifanyika jijini Dodoma – Mei 3.

Kwamba madeni haya yanaongezeka badala ya kupungua inatoa taswira fulani isiyopendeza kuhusu msimamo wa serikali katika jambo hili.

Siyo kwamba serikali haijui kuwa vyombo vingi vya habari vipo kwenye hali ngumu kiuchumi, la hasha! Tunakumbuka miezi kadhaa iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan aliunda tume mahsusi kuangalia suala la uchumi miongoni mwa vyombo vya habari.

Tume hiyo imekamilisha kazi yake na kufikisha ripoti kwa aliyeiunda.

Inafikirisha kidogo kuona kuwa kwa upande mmoja, serikali inaunda tume baada ya kuguswa na hali mbaya ya kiuchumi miongoni mwa vyombo vya habari, lakini kwa upande mwingine bado watoto wa serikali hiyohiyo ndio wanaoongoza kuvikopa vyombo vya habari na serikali haionekani kuchukua hatua madhubuti kukabili hali hiyo.

Sijui kama katika ripoti ya tume hiyo suala la madeni ya serikali kwa vyombo vya habari limeguswa, lakini binafsi ninaamini kuwa iwapo serikali ingeamua kulipa madeni yote ya vyombo vya habari, basi labda isingefika hatua ya Rais Samia kuona haja ya kuunda tume hiyo.

Ninamini pia kuwa mchango wa vyombo vya habari katika mchakato wa maendeleo na mambo mengine nchini ungekuwa mkubwa sana iwapo serikali ingekuwa inalipa madeni haya kwa sababu uwezo wa vyombo vya habari na waandishi wa habari kuzifanya kazi zao ungeimarika zaidi.



*Wasiri wa Habari, Nape Nnauye*

Pia ninaamini kuwa serikali ina uwezo wa kulipa madeni haya kwa sababu imeshafanya hivyo mahali pengine.

Serikali hii hii imeshawalipa wakandarasi na watoa huduma wengi ambao walikuwa na madeni makubwa kwa serikali kuliko haya ya vyombo vya habari.

Kinachonishangaza ni kwanini serikali haitaki kufanya hivyo kwa vyombo vya habari?

Ni kweli takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha hali ya uhuru wa vyombo, lakini takwimu hizo zisitudanganye tukadhani kuwa vyombo vya habari nchini vinafanya kazi katika mazingira mazuri.

Kuboreshwa kwa sheria hizo ni kweli zinaweka mazingira mazuri zaidi ya waandishi na vyombo vya habari kufanya kazi, lakini katika mazingira ya ukata, siyo rahisi kwa waandishi na vyombo vya habari kufanya kazi zao kwa ufanisi na kuleta tija inayotarajiwa.

Ni kama vyombo vya habari ambavyo sasa vinafanya kazi kwenye mazingira huru zaidi, lakini kwa sababu havina uwezo kiuchumi, haviwezi kufanya kazi zake kwa ufanisi licha ya uhuru unaonekana kuwepo.

## Habari

## Bunge: Serikali inahujumu kilimo

Na Mwandishi WETU  
Dodoma

**B**UNGE la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limebaini kuminywa kwa bajeti ya sekta ya kilimo, hatua iliyolinganishwa na hujuma.

Kupitia Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Bunge limekasirishwa na hatua ya serikali kutoa asilimia 15 tu ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka 2023/24.

Hatua hiyo imeelezwa na wajumbe wa kamati hiyo kuwa jambo hilo ni kama hujuma kwa sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya kilimo nchini.

Katika bajeti ya mwaka 2023/24, tume hiyo ilikuwa imetengewa kiasi cha Shilingi bilioni 73.547 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, lakini hadi kufikia Februari mwaka huu, serikali ilikuwa imeipatia tume hiyo kiasi cha Shilingi bilioni 11.364 tu, sawa na asilimia 15 fedha iliyoidhinishwa.

“Mwenendo huu wa upatikaji wa fedha hauridhishi na hautoi mwelekeo wa ukamilishaji wa lengo lililokusudiwa.

Miradi mingi ya umwagiliaji imeathirika kutokana na upatikanaji wa fedha usioridhisha,” inasema taarifa ya kamati hiyo iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita baada ya kuwasilishwa kwa Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Hali kama hiyo imejitokeza pia kwenye bajeti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika ingawa huko kuna nafuu kidogo.

Kwa mujibu wa taarifa ya kamati, tume hiyo ilidhinishwa jumla ya Shilingi bilioni 17.383 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, lakini, hadi kufikia Februari, 2024, tume ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 9.121 pekee sawa na asilimia 46 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa.

“Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hauridhishi na hivyo unaonyesha kwamba utekelezaji wa



Wasiri wa Kilimo, Hussein Bashe

malengo unaweza usifikiwe kikamilifu,” inasema taarifa hiyo iliyofika mezani kwa Pambazuko.

Kwa upande mwingine, kamati hiyo ilionyesha kutorishishwa na ukusanyaji wa mapato uliofanywa na wizara kwa mwaka wa fedha unaomalizika mwishoni mwa Juni mwaka huu.

Kamati ilibainisha katika taarifa yake kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, wizara ilijiweka lengo la kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 6.77, lakini hadi kufikia Februari mwaka huu, ilikuwa imekusanya bilioni 4.558 sawa na asilimia 68 ya lengo.

Ingawa hali hiyo ni ya kuridhisha, kamati ilibainisha kuwa ukusanyaji huo pia unaweza kumaanisha kuwa makadirio ya maduhuli yalifanyika chini ya kiwango.

Kwa upande wa Tume ya Umwagiliaji, kamati ilibainisha kuwa kwa mwaka wa Fedha 2023/24 ilijiweka lengo la kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 10.

Hata hivyo, kamati inasema kuwa hadi kufikia Februari mwaka huu, kiasi cha shilingi bilioni 1.7 pekee ndicho kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 17 ya lengo.

“Makusanyo haya hayaendani na matarajio na lengo la wizara, kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa asilimia 75

## **Bunge: Serikali inahujumu kilimo**

### **Inatoka Uk. 18**

ya muda wa utekelezaji umeshapita,” inaeleza kamati hiyo.

“Mwenendo huu wa makusanyo unaleta shaka kwenye makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli iwapo ulikuwa na uhalisia, aidha, mwenendo huu wa makusanyo unaweza pia kuashiria ukosefu wa mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa maduhuli na usimamizi wake,” imeendelea taarifa hiyo.

Katika maoni yake ya jumla, kamati hiyo inabainisha kuwa pamoja na serikali kuongeza bajeti kwa wizara ya Kilimo, lakini inaonekana kiasi cha nyingeza hakikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014), linalozitaka za Afrika, na hasa wanachama wa

Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kutenga asilimia 10 ya bajeti ya taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo.

Pamoja na kuongeza kiasi cha bajeti, kamati iliishauri serikali pia fedha hizo zitolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa.

Kamati imebainisha kuwa uzalishaji duni na usio na tija wa mazao ya kilimo, unatokana na kukosekana kwa mbolea ya kutosha na kwa wakati na hivyo kuishauri serikali kuweka nguvu na kuchukua hatua za makusudi kuzalisha pembejeo hapa nchini ikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu.

“Pamoja na serikali kuweka mfumo mzuri wa utoaji wa mbolea ya ruzuku

nchini, bado mfumo huo haujafahamika ipasavyo kwa wakulima wengi, hivyo kutoleta tija iliyokusudiwa,” inabainisha Kamati hiyo ya bunge.

Kamati ikaitaka wizara kuongeza idadi ya maofisa ugani ambao ni muhimu ili kukuza tija katika sekta hiyo muhimu.

Takwimu zilizopo, Tanzania inahitaji maofisa ugani 20,000, lakini waliopo ni asilimia 35 tu ya mahitaji.

### **Bajeti yenyewe**

Akiwasilisha bajeti hiyo awali, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aliliomba Bunge kuidhinisha kiasi cha Shilingi bilioni 824.069 zikijumuisha shilingi bilioni 700.318 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 123.750 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Bashe alisema kipaumbele kikubwa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka ujao ni kuongeza tija na uzalishaji katika sekta hiyo inayoajiri watu wengi nchini.


“Kipaumbele hiki hakibadiliki, lakini mikakati ya utekelezaji wake inaweza kubadilika,” alisema Bashe.

Alikitaja kipaumbele cha pili kuwa ni kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo, huku msisitizo wa tatu ukiwa ni kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

Kipaumbele cha nne katika bajeti hiyo ni kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi, wakati kipaumbele cha tano ni kuimarisha maendeleo ya ushirika, huku cha sita kikiwa ni kuimarisha matumizi ya mifumo ya Tehama katika uendelezaji wa Sekta ya Kilimo.



# Chui mweusi...



Mara nyingi, chui wanaofahamika kwa wengi ni wale wanaopatikana zaidi Afrika na maeneo mengine yenye uoto wa savannah. Hawa wana rangi ya njano na madoa meusi. Lakini kumbe chui wengine wapo. Hawa wana rangi ya kijivu na madoa meusi. Inaelewa kuwa wanapatikana zaidi Pakistan na kwamba wako hatarini kutoweka. Idadi yao inakadiriwa kuwa hati ya 4,000 hadi 6,500. (Picha kutoka WF).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

